## "URAHISI WA KUFANYA BIASHARA"





BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business. let's make it easy
Ukurasa huu unadhaminiwa na BEST-AC na Mwananchi

Kinamama wakiandaa maziwa tayari kwa kupeleka sokoni. Picha na Maktaba

# Mabadiliko ya kisera yatazuia anguko la sekta ya maziwa

Na **Veneranda Sumila**

UFANISI katika sekta ya maziwa nchini Tanzania ni mdogo ikili nganishwa na idadi halisi ya mi fugo iliyopo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, Tanzania ni ya pili kwa kuwa na mifugo mingi barani Afrika. Pamoja na ukweli huo, sekta ya maziwa ipo katika hatari ya kuanguka kama hatua za dharura hazitachukuliwa.

Kwa miaka mingi, sekta ya maziwa nchini imekuwa haina mchango wa kutosha kwa jamii, na badala yake sehemu kubwa ya mahitaji yanategemewa kutoka Kenya, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini. Ni dhahiri, maziwa yanayosindikwa nchini hayatoshelezi mahitaji ya Taifa.

Gharama za kufanya biashara kwa wasindikaji wa maziwa nchini ni kubwa kulinganisha na maziwa yanayoagizwa kutoka nje. Kutokana na mazingira hayo bei ya maziwa yanayosindikwa Tanzania ni sawa na yale yaliyoingizwa kutoka nje.

### Sera zibadilishwe

Chama cha Wasindikaji Maziwa nchini (Tampa) kinaamini kwamba kubadilisha sheria na taratibu kutasaidia sekta hiyo, kufunguka inavyopaswa na kuleta faida kwa taifa.

Serikali inapoteza takribaniSh13 bilioni ambazo zingetokana na kodi kila mwaka huku wafanyakazi 9,600 wanapoteza kazi kila mwaka katika sekta hiyo.

Utafiti umebainisha kwamba kama nusu ya lita za maziwa bilioni 1.65 zitasindikwa kila mwaka, sekta hiyo itatengeneza nafasi za kazi 76,577 na taifa litafanikiwa kuvuna Sh20.4 bilioni kila mwaka.

Kwa mujibu wa taarifa ya Tampa yenye kichwa cha habari: 'Uboreshaji wa ushindani kwenye sekta ya maziwa kupitia taratibu na sheria.' Kwa kufanya mabadiliko hayo kutaiondoa Tanzania katika pato la Sh800 milioni ambalo ni dogo kulinganisha na hali halisi ya kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo ili Watanzania wasindike angalau nusu lita bilioni 1.65 za maziwa, kuna masuala manane ya kuzingatiwa.

Katika sera yanapaswa kutazamwa na kubadilishwa:

Mkurugenzi Mtendaji wa Tampa Edmund Malick anasema Serikali ni lazima ichukue uamuzi mgumu kuangalia vikwazo katika ukuaji wa sekta hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ipo haja ya kuiwezesha Bodi ya Maziwa nchini (TDB), kusimamia, kutekeleza kanuni na sheria kuhusu sekta hiyo ili ikue.

"Haya yanaweza kufanywa kwa kuongeza bajeti, kuwa na wafa nyakazi wanaostahili," anasema Malick.

Malick anasema udhibiti uliowekwa na Serikali katika sekta hiyo unafaa kuondolewa na badala yake kanuni zinazotawala masuala ya chakula zishike mkondo wake.

Wakati wa kipindi cha mvua, wafugaji wanazalisha maziwa mengi, lakini mengi yanamwagwa kutokana na kukosekana kwa viwanda vya kusindika maziwa.

Meneja Mkuu wa kiwanda cha maziwa cha Tanga, Michael Karatu amesema kukosekana kwa mfumo wa kukusanya maziwa kutoka kwa wafugaji nchini kumesababisha maziwa mengi kumwagwa.

"Kama miundombinu itaandaliwa rasmi kutachochea kampuni binafsi kuwekeza katika usindikaji wa maziwa," amesema.

Tujadiliane kupitia ujumbe mfupi wa SMS na 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako.
Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi!

### Ugumu wa kufanya biashara

Wingi wa leseni zinazotakiwa kutoka TDB kwa ajili ya jengo, na kibali kwa kila bidhaa kutoka Shirika la Viwango (TBS) achi lia mbali leseni na vibali vingine kutoka BRELA, OSHA na mahitaji mengine.

Kuna ukaguzi mara tano kwa ajili ya jengo ili kutekeleza sheria tofauti kwa mfano, Sheria ya chakula, dawa na vipodozi ya mwaka, 2003, kifungu cha 5 (2) (f), Sheria ya viwango ya mwaka 2009, kifungu cha 4 (2) (b), Sheria ya viwanda vya kusindika maziwa ya mwaka 2004 kifungu cha 10 (r), (s), Sheria ya afya na usalama ya mwaka 2003, vifungu vya 24 (1) – (4) na 64 (3).

Tatizo la majaribio yasiyoratibiwa kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kuzingatia sheria zilizopo za chakula, dawa na vipodozi ya mwaka 2003.

**TAARIFA ZAIDI**

- Kuna ng'ombe wa maziwa 680,000 wenye uwezo wa kuzalisha lita bilioni 1.65 kila mwaka
- Sekta ya maziwa inachangia asilimia 30 ya pato la taifa.
- Sekta hiyo imeporomoka kwa asilimia 80 katika kipindi cha miaka 15 iliyopita.
- Nafasi za kazi 76, 577 na kodi inayofikia Sh 103 bilioni zinapotea kila mwaka kutokana na ku shindwa kusindika maziwa angalau nusu ya maziwa yanayoza lishwa nchini.
- Gharama za kutekeleza mabadiliko kwa sasa ni Sh 48 milioni kwa sababu sekta hiyo ina wadhibiti 15, inalindwa kupitia sheria 25 na inaendeshwa kwa kanuni 25.

### Tunatakiwa kuleta ushindani katika sekta ya maziwa

Kuna sheria na kanuni kadhaa zinazokwamisha ushindani na uwekezaji katika sekta hiyo ambazo zinatakiwa kurekebishwa na kuwekwa pamoja kupunguza usumbufu na kuongeza ufanisi.

i) Kuanzishwa kwa mpango wa kuratibu ukaguzi kwa pamoja kwa kuangalia kanuni za TFDA, TBS, TDB, Afya na usalama wa wafanyakazi (Osha).

ii) Kuanzishwa kwa majaribio ya pamoja ya bidhaa kwa mujibu wa kanuni za TFDA, TBS na TDB ili kupunguza usumbufu, kuokoa muda na gharama.

iii) Kupunguza msururu wa leseni na vibali kwa sheria za sasa kwa kuwa kiwanda kinachosindika maziwa hivi sasa kinapaswa kuwa na leseni 15 kwa ajili ya jengo na gari), na leseni hizo zinapaswa kukatwa kila mwaka .

iv) Kuwapo kwa maelezo ya kina ni vipi ukaguzi unapaswa kufanywa.

v) Mfumo wa sheria zilizopo zinapaswa kubadilishwa katika usindikaji maziwa ili kutoa mwanga wa uwajibikaji.

vi) Kuanzisha taratibu za wazi kwa mamlaka za Serikali zina zowajibika kwenye sekta ya maziwa kwa kuwa kutokuwapo kwa uwazi katika biashara kunachochea vitendo vya rushwa.

**Sh13 bilioni**

Fedha ambazo serikali ingekusanya kila mwaka.

**Sh20 bilioni**

Kiasi cha fedha ambacho kipo hatarini kupotea katika sekta ya maziwa nchini.